


Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.

Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenyi hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana(umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

 soundcloud.com/user-740750674
 Facebook.com/komaebola
 @Ebolakoma
 koma-ebola.info



EBOLA

SWALI

Ju ya nini mu ma hopitali saa banafanyaka ma examens habaongezake kwa limoya ma examens za Ebola pahali ya kungoya kuzifanyisha tu saa mutu alisha kufa?

JIBU

Kufanyisha mutu mwenyi anagonjwa ma examens za Ebola inafuatana na ma alama za ugonjwa zenyi zina muonekana ako.

Kama ma alama hazifanane za Ebola, examen haifanyiwe hapo hapo.

Lakini sasa, ju ya vifo vya kijamii, bila kuangalia hata sababu ya kifo, inaomba bafanye examen kwa kuweza kuhakikisha kama haiko Ebola.

Ma examens za ma echantillons ku maiti ni za batu tu benyi biko na ma alama za Ebola na vifo vya kijamii, lakini haiko ku batu bote benyi banagonjwa benyi banafika ku hopitali.

CORONAVIRUS

SWALI

Ni kweli batoto habiko banakamatika na Virusi ya Corona ju maziwa ya mu kifua ya mama njo dawa ya kweli ya Virusi ya Corona?

JIBU

Hapana, batoto nabo banaweza kamatika na COVID-19. Banashauri batoto baendeleye bananyonya kwa kuongeza kingo mwilini na kuweza kukomala.

Hata kama maziwa ya mama inaweza kinga watoto wachanga ku maambukizi za mingi, hakuyakuwa habari za kutosha zenyi kuelekea COVID-19 kuhusu batoto. Virusi ya Corona ikiwa virusi ya mupya, wanasayansi wangali na bya mingi bya kugunduwa kuhusu ile virus.

Mpaka hapo, hakuna hata dawa moyo ya kutunza COVID-19, matunzo ya leo inafuatana na ma alama zenyi mgondjwa iko nazo. Kwa hiyo inashauriwa kuheshimia na kuendelea kushika hatua za kujikinga kwa kuepuka na kukiinga batoto na COVID-19.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



**TRANSLATORS
WITHOUT BORDERS**

**PAUL G. ALLEN
FAMILY FOUNDATION**



Internews
Local voices. Global change.





EBOLA

SWALI

Tunasikia kama mu mingini zingine bamepana vituo vya matunzo ya Ebola (CTE) ku vituo vya afya na ma hopitali. Sasa huku kwetu bitakuwa siku gani? Ao muko munataka kuleta tena kesi ingine ya Ebola?

JIBU

Ma kesi za Ebola haziko za kujitungia. Ebola ni ugonjwa ya kweli na ni ya lazima ku jamii yote kujikinga nayo hata kama banafunga ma kazi za vituo vya matunzo ya Ebola (CTE).

Mpango ya baada ya riposte ya kupiganisha Ebola ina maana ya kuimarisha mfumo wa afya na nguvu ya kijamii kwa kuwapatia uongozi wa afya Jimboni na maeneo za afya kwa kuendelesha ma kazi za riposte (uchunguzi, na mawasiliano).

Na ni mwa ile nia njo vituo vya matunzo ya Ebola (CTE) vimoja vilifungwa ao kutiwa kwenyi uongozi ya ma hopitali ao ya vituo vya afya.

CORONAVIRUS

SWALI

Ju ya nini ma fasi za kunawiya mikono haziko hapa kwetu Biakato saa vile ilikuwaka wakati ya Ebola? Virusi ya Corona ayo haiambukiaka kupitia mkono?

JIBU

Namna yenyi bakubwa ya inchi balitia kwa kupiganisha COVID-19 ni namna ya kijamii. Njo maana, kunawa mikono inapashwa kuwa sawa kazi ya kila mutu yenyi inafanyika pia ndani ya kila jamaa.

Kama bale benyi balikuwa banaunga jamii mkono bakibapatia fasi ya kunawia mikono hababifanye tena, jamii inaombwa kuendelea kujikinga ayo pekee kuanzia kunawa mikono mara kwa mara.

Virusi ya Corona inaambukiaka kutokeya mutu umoja mpaka ku mutu mwengine, haiko tu kupitia matoni za maji za kupitia njia ya kupumulia wakati mtu anasema, ao saa anakohoaa ao anapiga chafya.

Inaweza ambukia saa moyo kutokeya mutu umoja mpaka ku mtu mwengine, na tena ukigusa kitu kyenyi kilisha ambukizwa. Manake mutu anawenza pata COVID-19 kama anagusa bitu ao zile fasi na kisha kama mutu anajigusa tena ku macho, ku puwa ao ku kinywa.

Njo kusema inaomba kunawa mikono saa yote na muzuri tukitumia maji ya kutakata na sabuni ao na désinfectant inayo kuwa na alcool....

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID).

Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

